






TAARIFA ZA HARAKA KUHUSU Essential Plan

MAPYA KATIKA
2021:
MALIPO YA BIMA YA
\$0 NA BIMA ZOTE
ZINAJUMUISHA
MACHO NA MENO.

Je, nitajisajili vipi?

 nystateofhealth.ny.gov
AU

 1-855-355-5777 au
TTY: 1-800-662-1220
AU

 Kupitia usaidizi wa ana
kwa ana wa bila malipo
kutoka kwa msaidizi
aliyeidhinishwa karibu
na nyumbani au kazini
kwako.

Je, mnaweza kunisaidia kwa lugha yangu binafsi?

Usaidizi unapatikana kwa
lugha yako kwa simu na ana
kwa ana.

Ninaweza kujiandikisha lini?

Usajili kwa Essential Plan
uko wazi mwaka mzima.

NY State of Health inazingatia sheria za haki za raia za Shirikisho zinazotumika na haibagui kwa msingi wa mbari, rangi, asili ya taifa, dini, jinsi, umri, hali ya ndoa/familia, rekodi za kukamatwa, hukumu za uhalifu, utambulisho wa jinsia, mwelekeo wa kingono, sifa za kinasaba, hali ya jeshi, hali ya mhanga wa unyanyasaji wa nyumbani, na/au kulipiza kisasi.

Je, Essential Plan ni nini?

Bima ya afya kwa Wakazi wa jimbo la New York isiyo na malipo kwa wale wanaostahiki. Na inatoa manufaa sawa yaliyo msingi.

Je, ni nani anaweza kuinunua?

Watu wenye mapato madogo zaidi ambao hawahitimu kupata Medicaid au Child Health Plus.

Ukubwa wa kaya	Pato la juu zaidi unaloweza kupata
1	\$25,760
2	\$34,840
3	\$43,920
4	\$53,000

Je, inagharimu nini?

Malipo ya bima ya kila mwezi ni \$0 kwa wale wanaostahiki.

Je, ni vipi vingine inavyo niokolea pesa ?

Haina DEDUCTIBLE (PUNGUZO), kwa hivyo mpango huu unaanza kulipia huduma yako ya afya mara moja.

Fidia za meno na macho zimejumuishwa bila uchangiaji wa gharama.

Unapata HUDUMA YA UZUILIAJI BILA MALIPO kama vile chunguzi na kaguzi za daktari za mara kwa mara ili kukuweka mwenye afya.

Je, Essential Plan inashugulikia nini?

Huduma sawia zinazotolewa na bima nyingine, ikijumuisha:

- kumwona daktari, ikijumuisha madaktari bingwa
- vipimo vilivyoagizwa na daktari wako
- dawa za kuandikiwa na daktari
- huduma za wagonjwa wa kulazwa na wa kurudi nyumbani katika hospitali na zaidi